# HATUA 5 ZA LAZIMA

KATIKA

## MRADI WA KUKU WA KIENYEJI

**“Maamuzi Muhimu Yatakayoepusha Usipoteze Pesa Zako.”**



- Matumizi ya MKEKA Katika Kudhibiti Magonjwa Korofi ya Kuku.
- Gundua Zaidi ya Aina 30 Adimu za Kuku wa Kienyeji Zenye Faida.
- Mtindo wa Ufugaji wa Kivivu Lakini Una Faida.
- Siri ya Kuuza Bei Yoyote kwa Mtu Yeyote.

MUJAYA JONES MUJAYA

# HATUA 5 ZA LAZIMA KATIKA MRADI WA KUKU WA KIENYEJI

# HATUA 5 ZA LAZIMA KATIKA MRADI WA KUKU WA KIENYEJI

"Maamuzi ya Muhimu Yatakayoepusha Kupoteza Pesa Zako"

# HATUA 5 ZA LAZIMA KATIKA MRADI WA KUKU WA KIENYEJI

"Maamuzi ya Muhimu Yatakayoepusha Kupoteza Pesa Zako"

**Mwandishi:** Mujaya Jones Mujaya
S. L. P 45019 Dar es Salaam,
Tanzania.

**Simu:** +255715678122 au +255768678122

**Barua Pepe:** ev.mujaya@gmail.com

**Mitandao ya Kijamii**: mujaya mj *(Instagram, Facebook, Telegram na Twitter)*

# HAKI MILIKI

Maandishi, mpangilio na usanifu wa kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Haki zote kuhusu kitabu hiki zipo chini ya **Mujaya Jones Mujaya.**

Haki zote zimehifadhiwa.

Ni marufuku kuzalisha, kudurufu, kusambaza, kunakili au kutumia sehemu yoyote ya maudhui ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na hatua kali za kisheria ikiwemo kifungo na faini zinaweza kuchukuliwa.

**© 2022**

# TABARUKU (DEDICATION)

Nimeandika kitabu hiki kiwe mahsusi kwa watu wote ambao wanafuga au wanatazamia kuanza kufuga kuku wa Kienyeji ili wajue mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wanaanza na kuendeleza mradi wao ili wajipatie faida endelevu.

Kitabu hiki kikawe hazina ya maarifa kichwani kwako na kikakupe pesa mfukoni mwako kupitia mradi wa ufugaji wa kuku wa kienyeji.

# SHUKRANI

Ninamshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kuandika kitabu hiki. Hatua zote nilizopita nimeona nyayo zake zimetangulia mbele yangu kunionesha njia na kuniwezesha.

Ninatoa shukrani za pekee kwa wote ambao wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha makala na vitabu hivi vinafika mikononi mwa walengwa.

Shukrani ziende pia kwa Bw. Peter James Mkandi, anayefanya kazi kubwa ya usanifu wa miradi yangu pamoja na Kuku Makini.

Bado ninadaiwa shukrani na familia yangu kwa kipindi kirefu nilipolazimika kujitenga kwa ajili ya kazi hii. Najua mnanijali nami ninawapenda sana.

Asante sana.

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| HAKIMILIKI | i |
| TABARUKU | ii |
| SHUKRANI | iii |
| YALIYOMO | iv |
| UTANGULIZI | 1 |
| MASOKO | 3 |
| UCHAGUZI WA KUKU | 9 |
| ELIMU YA UFUGAJI | 24 |
| MFUMO WA KUFUGA | 29 |
| AFYA – ULINZI WA VIUMBE HAI | 41 |
| HITIMISHO | 47 |
| MAWASILIANO MUHIMU | 50 |
| VITABU VINGINE VILIVYOANDIKWA | 51 |
| KUHUSU KUKU MAKINI | 53 |
| WASIFU WA MWANDISHI | 55 |

# UTANGULIZI

Utaepuka hasara nyingi endapo utajua unatakiwa kuanzia wapi kwenye mradi wako wa kuku wa kienyeji. Kujua unapotakiwa kuanzia kutakupatia fursa ya kuweka msingi imara wenye mizizi ya kina ili kukuhakikishia faida kwa kipindi kirefu.


Kabla haujaanza mradi wa kuku wa kienyeji unatakiwa kufuata hatua kuu tano ambazo lazima uzitekeleze kabla hata haujajenga banda au kununua kuku. Hatua hizi ni muhimu sana kwani zitakuhakikishia mavuno bora ya kutosha kutoka katika mradi wako. Hatua hizo ni *‘MKEKA’*.

*‘MKEKA’* unafahamika sana katika jamii nyingi za kiafrika kama kitu kinachotumika kutandika chini kwenye sakafu au kitanda kisha watu wanakaa au wanalala juu yake. Mkeka hutumika kuketi kwa ajili ya chakula, kulala, kupumzika, kupiga soga, kufanya ibada, shughuli za mazishi na mapambo ya nyumbani.

Kwa kifupi *‘MKEKA’* unatumika kama kitu ambacho kinakaa chini kabisa na shughuli nyingine au huduma zinafanyika juu yake. Katika maana hii *‘MKEKA’* ni msingi na mambo mengine yanajengwa au yanatendeka juu yake.

HATUA YA KWANZA

# MASOKO



**Epuka Kosa Hili!**

Miongoni mwa makosa makubwa ambayo wafugaji wanafanya ni kuanza kufuga bila kujua watauza wapi bidhaa zao. Wengi wamelizwa na madalali kwa bei za chini sababu hawakujua soko kabla ya kuanza ufugaji.

Walanguzi wanaweza kukupa 'stress' hadi ukachanganyikiwa. Watakwambia kuku hawanunuliki hivyo uza kila kuku kwa bei yao. Kama haujajipanga utajikuta umeliwa. Kwako anamnunua kuku wa kienyeji Tshs. 8,000 kisha anaenda kumuuza ambako haupajui Tshs. 15,000. Yani mlanguzi anapata faida mara 100 kukuzidi wewe uliyeteseka na kuku.

HATUA YA NNE

# MFUMO WA KUFUGA



Baada ya kuamua na kuchagua mbegu ya kufuga hatua inayofuata ni kuchagua mfumo wa kuwafuga kuku wako. Maamuzi haya unatakiwa kuyafanya kabla haujaanza kujenga banda wala kununua kuku. Uchaguzi wa mtindo wa ufugaji unategemea rasilimali zilizopo kwajili ya biashara hasa fedha, ardhi, wafanyakazi na teknolojia.

Mambo ya msingi yanayomfanya mfugaji kuamua atumie njia fulani ya kufuga ni pamoja na uwezo wa kugharamia shughuli ya ufugaji wa kuku na ukubwa wa eneo alilonalo la kufugia. Mitindo ya ufugaji wa kuku humaanisha mifumo mbalimbali ya ufugaji wa kuku.

HATUA YA TANO

# AFYA: Ulinzi wa Viumbe Hai



Baada ya kuchagua mfumo wa kufuga kuku wako unatakiwa kufanya maamuzi ya jinsi kulinda afya za kuku utakaowafuga ili wasipate magonjwa kwa urahisi. Maamuzi ya mbinu za kudhibiti magonjwa ni mkakati ambao unatakiwa kuwepo hata kabla haujaanza kufuga wala kujenga banda.

Njia sahihi ya kupambana na magonjwa ni kukinga yasitokee. Kwahiyo unatakiwa kuwa na mpango wa kujikinga na magonjwa mapema kabla haujaanza lolote kwenye mradi wako.

# HITIMISHO

Uendeshaji wa miradi ya kuku wa kienyeji ina faida kubwa sana na pesa nyingi ambazo unaweza kuzichangamkia na ukatoka chapchap.

Lakini ili unufaike na miradi hiyo unatakiwa kuwekeza kwa uangalifu, huku ukizingatia mbinu za kitaalamu katika kuzalisha na kuuza bidhaa zako.

Kitabu hiki kimekupatia mwanga tu hatua za awali kabisa unazotakiwa kuchukua kabla haujaanza kutumia pesa zako kwenye mradi. MKEKA ni kanuni ambazo ni msingi wa maamuzi yako yote yanayofata katika kuendesha na kusimamia mradi wa kuku wa kienyeji.

Kanuni hizi zitalinda mradi wako kwa kipindi kirefu ili uendelee kunufaika kwa kukwepa hasara na majanga ambayo yangekupata endapo usingezingatia kanuni.

Baada ya kufanya maamuzi kwa kuongozwa na MKEKA unatakiwa sasa uchukue hatua za kuanza mradi wako moja kwa moja.

Utahitaji kujua zaidi jinsi ya kutunza na kuendeleza mradi wako, unatakiwa kujua ujenzi wa banda bora, uzalishaji wa mayai, vifaranga na nyama bora, unahitaji

kujua magonjwa sumbufu na jinsi ya kuyatibu kirahisi, unatakiwa kujifunza mbinu za kulea vifaranga bila vifo, ujue jinsi yakutotolesha vifaranga wengi kwa mpigo, mbinu za kupambana na washindani wako kwenye soko, utunzaji wa kumbukumbu zako, ulishaji wa chakula bora kwa gharama nafuu n.k

Mambo haya ni mengi na hautakiwi kuyafahamu mambo hayo juu juu tu, kwakuwa faida na mafanikio yako yanategemea kina cha maarifa uliyonayo.

Kitabu hiki kimekuletea maarifa muhimu kuhusu hatua ambazo mfugaji mdogo anayeanza ufugaji anatakiwa kuzipitia. Kitabu kimejikita kuonesha kivitendo mambo ya msingi ambayo yanayotakiwa kufanyika ili kujihakikishia faida.

Hatua za MKEKA katika kitabu hiki yamejikita zaidi kwa kuku wa kienyeji japo kimsingi zinafaa hata kwa aina zingine za kuku wa kisasa au chotara. Ujuzi huu bado ni muhimu, ujuzi huu bado unaweza kutumika kwa aina nyingine za kuku.

Pamoja na mambo yote uliyojifunza, elimu hii bado ni ndogo, ni elimu ya msingi inayokusaidia kuanza na kuendesha mradi wako siku za awali. Ili ufike vilele vya juu unahitaji elimu ya kina zaidi hasa jinsi ya kusimamia

na kuendesha maeneo mbalimbali ya kimkakati kuhusu mradi wako.

Hivyo ikiwa unataka kufika uzalishaji wa kati au mkubwa wa kuku wa kienyeji unatakiwa upate vitabu vingine nilivyokuandikia vilivyojikita kwenye maeneo hayo ya kimkakati kama ambavyo utahitaji.

Ni imani yangu utawashirikisha watu wengine ujuzi huu na utautendea kazi. Ninakuombea baraka na mafanikio mema unapojikita katika shughuli zote halali za miradi ya ufugaji wa kuku.

## MAWASILIANO MUHIMU


**Mawasiliano ya Mwandishi:**

**Barua Pepe:** ev.mujaya@gmail.com
mujaya@kukumakini.co.tz

**Simu:** +255 768 678 122

**Instagram:** @mujaya_mj

**Facebook:** mujayamj

**Facebook Page**: Mujaya MJ (@kuku makini

**Telegram:** mujaya

**Twitter:** mujayamj


**Mahitaji ya Vitabu Vingine:**

+255 785 071 914

+255 653 113 103

+255 768 678 122

## VITABU VINGINE VILIVYOANDIKWA NA

## MUJAYA JONES MUJAYA

**Dawa za Asili za Kutibu Magonjwa Sugu ya Kuku**. *"Dawa zaidi ya 100 zilizo jirani yako; zitakazokuweka mbali na daktari wa mifugo daima."*

**Kwanini Nimekimbilia Kufuga Kuku?**

*"Jinsi yakushinda changamoto za ufugaji wa kuku kizembezembe."*

**Hauwezi Kusimamia? Bora Uache Kufuga Kuku.**

*"Jinsi ya kusimamia mradi wa kuku kwa mafanikio bila uwepo wako."*

**Fuga Kuku Bila Magonjwa**.

*"Siri za kutambua na kutibu magonjwa ya kuku kirahisi kama daktari wa mifugo"*

**Sahau Kabisa Vifo vya Vifaranga.**

*"Utasumbuliwa kwa magonjwa na vifo vya vifaranga hadi lini?"*

**Kila Kitu Kuhusu Chakula cha Kuku.**

*"Jinsi ya kuwalisha kuku chakula bora kwa muda mrefu bila gharama yoyote."*

**Nimefanya Hivi Tu, Yametotolewa Yote.**

*“Mbinu za Kutotolesha vifaranga wengi kama kiwandani wakati umelala usingizi”*

## Msingi Imara wa Ufugaji wa Kuku wa Kienyeji.

*“Jifunze mambo ya msingi kutoka kwa wafugaji waliofanikiwa ambayo wewe hauyazingatii.”*

## Ufugaji wa Kuku wa Kienyeji Kama Mradi

*“Hatua kwa Hatua Kuelekea Ufugaji wa Kuku wa Kienyeji Wenye Tija”*

## Pata Bei Nzuri Kwenye Masoko 101 ya Kuku.

*“Mwongozo wa jinsi ya kufanya biashara zinazohusika na kuku kiushindani.”*

## Banda la Kuku Makini.

*“Hakuna siri tena za ujenzi wa banda bora linalodumu miaka mingi kwa gharama nafuu.”*

## Kuku ni Pesa.

*“Msaafu wa kuku makini kuelekea ufugaji wenye tija na biashara zenye faida kubwa kutokana na kuku.”*

## Mali na Daftari

*“Jinsi Utunzaji wa Kumbukumbu Unavyoweza Kuongeza Faida na Mapato Katika Ufugaji wa Kuku.”*

KUHUSU

# KUKU MAKINI

Kuku Makini ni kampuni inayojishughulisha na utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalamu (Consultancy) kuhusu kusimamia na kuendeleza miradi inayojihusisha na kuku.

**HUDUMA ZETU**
Semina na Mafunzo.

**Ukaguzi wa Mashamba, Mabanda na Miradi** (Farm Audit) inayojihusisha na kuku ili kukupatia Uhakikisho na Ushauri kwamba umezingatia vigezo vya uendeshaji na usimamizi bora na kwamba utapata faida kwa kipindi kirefu.

**Ushauri wa kitaalamu** (Consultancy) kuhusu Ujenzi wa mabanda bora, usimikaji wa miundombinu ya ufugaji, Usimamizi wa Mtaji, Rasilimali watu na ajira, Fedha, Masoko pamoja na Udhibiti wa magonjwa.

**Uchambuzi wa miradi** ya kuku ili kutoa ushauri na kusaidia kwenye kupanua mradi, kuasili teknolojia mpya na kuboresha utendaji.

**Tathmini ya Mtaji** unaotakiwa kuanzisha na kuendeleza mradi wa ufugaji na biashara zinazohusiana na kuku. Tathmini hii ni muhimu kwa wanaoanza biashara au miradi, wanaotaka kupanua na kukopa. Kwa wanaokopa tahmnini hii itakueleza ukope kiasi gani na utafanyaje kulipa marejesho kwa wakati au kama unataka kuwekeza pesa zako mwenyewe uweke kiasi gani kulingana na malengo yako ya kibiashara.

**Uandaaji wa Taarifa za Mapato na Matumizi Pamoja na Taarifa ya Mizania** ili kubaini kama unapata faida au hasara kwenye ufugaji wa kuku na biashara zake.

## Mawasiliano

**Barua Pepe:** info@kukumakini.co.tz
**Tovuti:** www.kukumakini.co.tz
**Simu:** +255 714 261 609
**Whatsapp:** +255 768 678 122
**Telegram:** kuku makini
**Instagram:** @kuku makini
**Facebook:** OPOA (*Online Poultry Academy*)/@Kuku Makini Official

## WASIFU WA MWANDISHI



Mujaya Jones Mujaya ni mjasiriamali, mwandishi wa vitabu na Makala, mtafiti wa ufugaji wa kuku na biashara zake.

Alihitimu shahada ya Biashara katika uhasibu na usimamizi wa fedha kwenye biashara kutoka Chuo Kikuu Mzumbe.

Mujaya amewahi kufanya kazi kama Mkaguzi wa Hesabu (Auditor), Afisa Mikopo wa benki, Afisa Uendeshaji wa Benki, Mhasibu, Mtafiti na Mkaguzi wa Ndani (Internal Auditor).

Kwa zaidi ya miaka 10 amekuwa mtafiti na mshauri wa kitaalamu wa ufugaji wa kuku na kupelekea kuandika Vitabu na Makala ambazo zimebadilisha maisha ya wafanyabiashara na wafugaji wa kuku.

Vitabu vilivyoandikwa na Mujaya ni 14, vyote vinahusu ufugaji wa kuku na uendeshaji wa biashara zinazohusiana na kuku.

Makala maarufu zaidi aliyoandika ni “Ufugaji wa Kuku wa Kienyeji Kama Mradi” ambayo imesomwa na watu zaidi ya milioni 5, imepakuliwa (downloaded) na watu zaidi ya laki 5,

imeshirikishwa kwa watu zaidi ya laki 5 na imechapishwa kwenye blogu (blogs) zaidi ya 1000.

Mujaya amekuwa mkufunzi na mwezeshaji mbobevu kwenye majukwaa ya wajasiriamali, biashara na fursa za kujikwamua kiuchumi kwa zaidi ya miaka 10.

Ni mwanzilishi wa Kuku Makini, taasisi ambayo imelenga kuwasaidia wafugaji na wafanyabiashara zinazohusika na kuku ili wapate faida na kuona tija.

Mwandishi ni Mwadventista wa Sabato, na katika imani yake amehudumu kama muinjilisti, kaimu mchungaji, mzee wa Kanisa, mjumbe wa kamati tendaji za idara za jimbo, shemasi, mwenyekiti wa vyama vya wanafunzi kitaasisi na kikanda pamoja na kudumu kama mshiriki mwaminifu.

Uzoefu wake kwenye ufugaji wa kuku, uhasibu, ukaguzi, usimamizi wa fedha, benki na uongozi katika maeneo mbalimbali unakupatia mchanganyiko sahihi wa ujuzi na ufahamu unaotakiwa kupata kuhusu ufugaji wa kuku wenye tija na uendeshaji wa biashara za kuku kwa mafanikio.